

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**



**MKUTANO WA NNE**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO**

**13 SEPTEMBER, 2016**

## **MKUTANO WA NNE**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO - TAREHE 13 SEPTEMBER, 2016**

### **I. DUA:**

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Dkt. Tulia Akson, Naibu Spika ilisoma Dua na kuongoza Bunge.

### **MAKATIBU MEZANI:**

1. Ndg. Lawrence Makigi
2. Ndg. Lina Kitosi
3. Ndg. Zainab Issa

### **II. MASWALI:**

Maswali yafuatayo yaliulizwa:

#### **1. OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Swali Na. 56: Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye  
Nyongeza: Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye

Swali Na. 57: Mhe. Raphael Japhary Michael (liliulizwa na Mhe. Anthony Komu)  
Nyongeza: i) Mhe. Anthony Calist Komu  
ii) Mhe. Desderius John Mipata  
iii) Mhe. George Malima Lubeleje

Swali Na. 58: Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibajuka (liliulizwa na Mhe. Mendrad Kigola)  
Nyongeza: i) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola  
ii) Mhe. Pauline Philip Gekul

#### **2. OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Swali Na. 59: Mhe. Zubeda Hassan Sakuru (liliulizwa na Mhe. Pauline Philip Gekul)

Nyongeza: Pauline Philip Gekul.

Swali Na. 60: Mhe. Mussa Ramadhani Sima  
Nyongeza: Mhe. Mussa Ramadhani Sima.

#### **3. WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Swali Na. 61: Mhe. Boniface Mwita Getere  
Nyongeza: Mhe. Boniface Mwita Getere.

Swali Na. 62: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab  
Nyongeza: Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab.

4. WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na. 63: Mhe. Othman Omar Haji  
Nyongeza: Mhe. Othman Omar Haji.

Swali Na. 64: Mhe. Fatma Hassan Toufiq  
Nyongeza: Mhe. Fatma Hassan Toufiq.

5. WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na. 65: Mhe. Susan Peter Maselle  
Nyongeza: Mhe. Susan Peter Maselle.

Swali Na. 67: Mhe. Hasna Sudi Kakunda Mwilima  
Nyongeza: Mhe. Hasna Sudi Kakunda Mwilima.

6. WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Swali Na. 68: Mhe. Edward Franz Mwalongo  
Nyongeza: Mhe. Edward Franz Mwalongo.

7. WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Swali Na. 69: Mhe. Cosato David Chumi  
Nyongeza: Mhe. Cosato David Chumi.

Swali Na. 70: Mhe. Angelina Adam Malembeka  
Nyongeza: Mhe. Angelina Adam Malembeka.

**III. MATANGAZO:**

1. Wageni mbalimbali waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na kuona namna Bunge letu linavyofanya kazi walitambulishwa.
2. NIDA – wamekamilisha utengenezaji wa vitambulisho vya Waheshimiwa Wabunge hivyo wakavichukue Ukumbi wa Msekwa na ambao hawajajiandikisha wakafanye hivyo.

**IV. MWONGOZO WA SPIKA:**

1. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na 46 alieleza kutoridhika na majibu ya Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani wakati wa kujibu swali Na. 66.

Mhe. Naibu Spika aliahidi kutoa Mwongozo baadaye baada ya kujiridhisha kwenye Hansard namna maswali yalivyoulizwa na yaliyojibiwa.

2. Mhe. John Wegesa Heche alitumia Kanuni ya 47 kuomba Shughuli za Bunge ziahirishwe ili kujadili jambo la dharura lililojitokeza Bukoba (Kagera) la tetemeko la ardhi ambalo limetokea huko na kusababisha maafa.

Naibu Spika alishauri kwamba kwanza Wabunge wasikilize kauli ya Wawaziri ili kuona kama kuna haja ya kufanya hivyo.

## **V. KAULI ZA MAWAZIRI:**

Kwa niaba ya Waziri Mkuu, Mhe. Simbachawene Waziri wa TAMISEMI alitoa kauli ya Serikali kuhusu maafa yaliyojitokeza Bukoba (Kagera)

Baada ya kauli hiyo Mhe. Shangazi alisimama kwa Kanuni ya 69(1) kuomba mjadala uahirishwe kwa dakika 30 ili Wabunge wachangie kidogo suala la tetemeko na maafa yaliyotokea huko na hoja ya kukatwa posho ya siku 1.

Mhe. Naibu Spika aliamua kutoa dakika 30 ili Waheshimiwa Wabunge wajadili hoja ya Mhe. Shangazi ya kukatwa posho ya siku 1. Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kujadili.

- |                                       |   |         |
|---------------------------------------|---|---------|
| 1) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi      | - | CCM     |
| 2) Mhe. Masoud Abdallah Salim         | - | CUF     |
| 3) Mhe. John Wegesa Heche             | - | CHADEMA |
| 4) Mhe. Zaynab Matitu Vullu           | - | CCM     |
| 5) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka | - | CCM     |
| 6) Mhe. Dkt. Charles John Tizeba      | - | CCM     |

Baada ya Mhe. Rashid Abdallah Shangazi kuhitimisha Hoja yake, Naibu Spika alilihoji Bunge kama wanakubali posho yao ya siku moja ya tarehe 13/9/2016 ikatwe kwenda kuwafaraji waliopatwa na maafa kwa mikoa iliyopata tetemeko la ardhi Hoja ambayo ilikubaliwa.

Mhe. William Vangimembe Lukuvi alipewa nafasi ya kushukuru kwa Wabunge kukubali kukatwa posho hiyo. Naibu Spika naye aliwashukuru Wabunge na kuagiza Serikali kufanya tathmini haraka na kwamba Serikali ilete taarifa za hatua zilipofikia katika kutatua matatizo ya Wahanga wa tetemeko la Ardhi.

## **VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

Majadiliano yaliendelea kwa Miswada ya Sheria ifuatayo:-

- 1) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 (*The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016*).
- 2) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (*The Chemist Professionals Bill, 2016*).

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliendelea kutoa michango yao:-

- |   |           |
|---|-----------|
| 16. Mhe. Benadetha Kasabago Mushashu    | – CCM     |
| 17. Mhe. Lucia Michael Mlowe            | – CHADEMA |
| 18. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab     | – CCM     |
| 19. Mhe. Richard PHILIP Mbogo           | – CCM     |
| 20. Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel      | – CHADEMA |
| 21. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege      | – CCM     |
| 22. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | – CHADEMA |
| 23. Mhe. Dkt. Elly Marco Macha          | – CHADEMA |
| 24. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla  | – CCM     |

Naibu Spika aliongeza muda ili Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangalla amalize hoja zake chini ya Kanuni ya 28(2) baada ya kuwahoji Wabunge.

## **VII. KUSITISHA BUNGE:**

Saa 7.10 mchana Naibu Spika alisitisha Kikao cha Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

## **VIII. BUNGE KUREJEA:**

Bunge lilirejea Saa 11.00 Jioni, na kuongozwa na Naibu Spika, mjadala wa Miswada ya Sheria ya Serikali uliendelea na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alijibu Hoja za Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia Miswada ya:-

- i) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016; na
- ii) Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016.

**IX. KAMATI YA BUNGE ZIMA**

Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima na kupitisha Muswada wa Sheria wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 (*The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016*) Ibara kwa Ibara.

Wakati wa Kamati, Bunge lilirejea kumruhusu Waziri kutengua Kanuni ya 28(4) ili shughuli za Bunge na Kamati ziendelee hadi zitakapokamilika.

Baada ya Kamati ya Bunge Zima kukamilisha kazi yake Bunge lilirejea.

**X. BUNGE KUREJEA:**

Bunge lilirejea na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alitoa taarifa na Bunge lilihojiwa na Muswada ulisomwa kwa Mara ya Tatu na kuupitishwa.

**XI. KAMATI YA BUNGE ZIMA:**

Bunge lilikaa tena kama Kamati ya Bunge Zima kwa ajili ya kupitisha ibara kwa ibara Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (*The Chemist Professionals Bill, 2016*).

**XII. BUNGE KUREJEA:**

Bunge lilirejea na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alitoa Taarifa na Bunge lilihojiwa na kukubali, Muswada ulisomwa kwa Mara ya Tatu na hivyo kuhesabika kupitishwa na Bunge.

Baada ya kupitishwa Miswada yote miwili, Mhe. Naibu Spika alitoa maelezo kuwa sasa Miswada hiyo itapelekwa kwa Mhe. Rais ili kupata kibali chake kwa mujibu wa Kanuni ya 92.

**XIII. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE**

Saa 5.23 usiku Mhe. Naibu Spika aliahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe 14/09/2016 Saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA  
13 SEPTEMBER, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**